*JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA*
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO**
*(BaruazotezitumwekwaMkurugenziMtendajiWilaya)*

Simu Na +255 (0) 262 965 824/5
Fax Na +255 (0) 262 965 825
ded@uramboc.go.tz
tovuti: www.urambodc.go.tz

**MkurugenziMtendaji(W)**
30 Br. ya StendiBoma,
45582 Urambo.
S.L.P 170 Urambo-Tabora.

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb.Na.UDC/W.1/254/VOL.1/74** Tarehe: **04/07/2022**

## TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo anapenda kuwatangazia watanzania wote walioomba nafasi ya kazi ya Mtendaji wa Kijiji Daraja la III, Katibu Mahsusi Daraja III na Dereva Daraja II zilizotangazwa kupitia Tangazo lenye Kumb.Na. UDC/W.1/254/VOL.1/73 la tarehe 25/05/2022 kuwa usaili unatarajiwa kufanyika tarehe 11/07/2022 hadi tarehe 15/07/2022 katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo kuanzia saa 07:30 Asubuhi. Ratiba ya usaili kwa kila kada iliyotangazwa itakuwa kama ifuatavyo;

| Na | Kada | Tarehe ya usaili wa mchujo | Tarehe ya usaili kwa Vitendo | Tarehe ya Usaili wa Mahojiano |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Dereva II | Hakuna | 11.07.2022 | 12.06.2022 |
| 2 | Katibu Mahsusi III | Hakuna | 11.07.2022 | 12.06.2022 |
| 3 | Mtendaji Kijiji III | 13.07.2022 | Hakuna | 14-15/07/2022 |

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia kwa walioitwa kwenye usaili huuu;**

i. Kila msailiwa aangalie jina lake kama lipo kwenye orodha ya wasailiwa kwa usahihi
ii. Kwa msailiwa aliyesoma nje ya Nchi ahakikishe vyeti vyake vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika.
iii. Kila msailiwa anapaswa kuwa na kitambulisho kwaajili ya utambuzi kama vile cha mpiga kura, kazi, NIDA au hati ya kusafiria.
iv. Kila msailiwa atajigharamia kwa chakula, usafiri na malazi

v. Kila msailiwa ambaye hatafika na nyaraka halisi (original) kama zilivyoainishwa kwenye tangazo la kazi hataruhusiwa kufanya usaili

vi. Waombaji kazi ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili watambue kwamba hawakukidhi vigezo. Hivyo wasisite kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa kwa kusoma vyema masharti ya kazi husika

vii. Pia mnashauriwa kutembelea tovuti ya Halmashauri www.urambodc.go.tz na mbao za matangazo ili kupata taarifa endapo kuna mabadiliko yatakayojitokeza.

3. Nawatakia kila la kheri.

*Baraka Michael Zikatimu*
**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**URAMBO**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P. 170
URAMBO

Nakala: Katibu Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320,
**DODOMA.**

TANZANIA
SENSA
23 Agosti
2022
Jiandae Kuhesabiwa

*JiandaekuhesabiwaSikuyaJumannetarehe 23*